

Salamu za kuaga mwaka na kukaribisha mwaka mpya

By SW - Melkisedeck Shine · July 11, 2016

Biashara - Mbinu za Ujasiriamali na Biashara Kufanya tofauti · #Karibu AckySHINE · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF · #Ujasiriamali: Mbinu za Kuwa Tajiri

KWAHERI MWAKA JANA. UMENIFUNZA MENGI.

Mwaka umefika mwisho, zimebaki siku tatu tu kuingia mwaka mwingine lakini yapo mengi niliyojifunza mwaka huu na pengine ningepesha kushare:

1. Kwamba si lazima sana kuwa na rundo la marafiki kama hawaleti positive effects kwenye maisha yako. Urafiki wa maongezi yasiyoleta maendeleo ni uzamani chakavu.
2. Matumizi madogomdogo yasiyo ya lazima hucheleweshwa maendeleo makubwa yenye kiu na mimi. Nmekuwa na matumizi yasiyo ya lazima na ndio matundu hayo madogo yamezamisha meli.
3. Mungu ndio kila kitu. Anza na maliza siku na Mungu. Ukikosacho hakukupangia, usiumie, muombe akuletee atakacho.
4. Harusi zinaumiza. Usipojiwekea kiwango maalum na idadi ya harusi za kuchangia kwa mwaka na kwa umuhimu utakuja kujenga nyumba kwenye harusi za wenzako.
5. Lawama ni muhimu sana ili maisha yaende, usiogope hasa pale unapokuwa unasimamia lililo la kimaendeleo kwako. Kumridhisha kila binadam ni ngumu. Kuna muda ni kwa maendeleo yako inabidi uwe mbinafsi.
6. Mapenzi ni mazuri ila yasikuzidi 'kimo', vipo vyamaana vya kulilia sio mapenzi. Kikulizacho ndicho ulichokipa kipaumbele. Mtu aamuapo kukuliza na wewe ukalia basi umemtukuza. Mapenzi yasiyosumbua na yaliyojaa mijadala ya kimaendeleo ndiyo mapenzi yenye afya.
7. Watu waliowengi hasa kwenye mitandao ya kijamii wana matatzo na ukichaa, usibishane nao hasa kwenye mambo yasiyokuletea wewe maendeleo. Usione hasara kuwafanya wajione washindi.
8. Wazazi ni Muhimu sana, sala zao ni muhimu kwako. Usipende kuhonga mpita njia akuachaye siku yeyote ukawasahau wazazi wako. Wapo watu sikukuu hizi wametumia maelfu ya shilingi kuhudumia wanawake zao au wanaume zao wapitaji wakasahau wazazi wao hata kwa pesa ya dawa.
9. Kuahirisha mambo ni ugonjwa wa kuridhika na dhiki. Uahirishapo atakaye uwe chini anafurahi. Muaibishe shetani kwa mipango thabiti.
10. Panga kwaajili ya MWAKA kabla haUjafika, kupanga kunakupa nafasi ya kujihakiki. Mpya mwaka wa kucheza na 'alternatives'.